# DISTINCTION SCHOOL BASED ASSESSMENT TEST

## DARASA LA NANE - 2020

## KISWAHILI: LUGHA

8 PREMIER

EDUCATIONAL DISTINCTION PUBLISHERS 002 QUALITY IS OUR CONCERN 002

*Muda: Saa 1 Dakika 40*

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Jaza kila pengo kwa kuchagua jawabu lifaalo zaidi.***

Kalulu alishangaa ___1___ azimie ___2___ na ujumbe wa kifo cha kaka yake. ___3___ kwa ndugu yake huyo kulitokana na ___4___ uliompata akiwa katika anasa. ___5___ alikanywa na wazazi pamoja na walimu, alikataa kabisa kusikia. ___6___ muda wake ___7___ akinywa pombe na kutumia mihadarati mingine. "Potelea mbali, hakuna haja ya kuhuzunika," Kalulu alijiambia. Alikuwa ameamini kuwa ___8___ .

1. A. nusura B. tangu C. hadi D. halafu
2. A. alipofikia B. alipofikiwa C. alipofikisha D. alipofika
3. A. Kufa moyo B. Kufa ganzi C. Kuaga dunia D. Kufa kikondoo
4. A. magonjwa B. maradhi C. ugonjwa D. ndwele
5. A. Ingawa B. Iwapo C. Lakini D. Hata
6. A. Aliyapoteza B. Alimpoteza C. aliipoteza D. Aliupoteza
7. A. wingi B. nyingi C. mingi D. mwingi
8. A. kifo cha wengi ni harusi B. ndugu ni kufaana si kufanana C. mwiba wa kujidunga hauambiwi pole D. akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki

Nilipofika langoni ___9___ pa shule yetu, ___10___ mwanafunzi mmoja akiingia ___11___. Niliendelea kutembea ___12___ kutokana na maumivu ___13___ mguuni. ___14___ siku hiyo ilikuwa ya ___15___ sikuwa na lingine ila kuenda shuleni.

9. A. ile B. pale C. kule D. mle
10. A. nilimwona B. nilikuona C. niliona D. niliwaona
11. A. kwenye darasa B. kwa darasa C. katika ya darasa D. darasani
12. A. ninachechemea B. nilichechemea C. nikichechemea D. nimechechemea
13. A. yaliyokidhi B. yaliyokithiri C. yaliyozimia D. yaliyopooza
14. A. Maadamu B. Mathalani C. Mingairi D. Aghalabu
15. A. kuukalia mtihani B. kujionea mtihani C. kuufanya mtihani D. kufanyiwa mtihani

***Kuanzia nambari 16 mpaka 30, chagua jawabu lifaalo zaidi.***

16. Chagua umoja wa;
**Vita huharibu mazingira yetu.**
A. Vita huharibu mazingira yangu.
B. Kita huharibu mazingira yetu.
C. Vita huharibu zingira yetu.
D. Kita huharibu zingira yangu.

17. Tambua jibu lenye vivumishi vya sifa pekee.
A. Chake, langu, wako
B. Wengi, vichache, kadhaa
C. Hili, hao, hivyo
D. bora, shujaa, mweusi

18. Tumia jibu sahihi kujazia nafasi.
**Mkononi ________ chaki mbili.**
A. mna B. pana
C. una D. ina

19. Chagua sentensi iliyo katika hali ya mazoea.
A. Mwanafunzi aandikaye vizuri ndiye yule.
B. Mgeni aliongea huku akitabasamu.
C. Wewe hukuwasili kazini mapema.
D. Darasa litakalopakwa rangi ni letu.

20. Sentensi gani iliyotumia kimilikishi cha nafsi ya tatu?
A. Mbwa wangu ametibiwa.
B. Pale njiani ndipo nilipoliona gari lako.
C. Kiongozi wenu si fisadi.
D. Nyumba yao ina mabati mapya.

21. Teua sentensi ambayo **si** sahihi kisarufi.
A. Rinda lile lingine limenunuliwa.
B. Mwalimu amenipa kalamu nyingine mbili.
C. Mbuzi mwengine amekunywa maji.
D. Kabati jingine lina vikombe vipya.

22. Panga nahau zifuatazo zinazohusu mahakamani kuanzia ya kwanza hadi ya mwisho.
***(i) Kata kesi***
***(ii) tia mbaroni***
***(iii) kula kalenda***
***(iv) kata rufaa***

A. (ii), (i), (iv), (iii) B. (iii), (iv), (i), (ii)
C. (i), (iii), (ii), (iv) D. (iv), (i), (ii), (iii)

23. Jibu lipi lililo na nomino za ngeli ya **U - YA** pekee?
A. Machura, makobe, mababu
B. Magari, matunda, meno.
C. Maradhi, mawazo, maumivu
D. Mapishi, malezi, magonjwa

24. Methali gani ambayo ni tofauti na zingine katika orodha hii?
A. Dua la mnyonge haliendi joshi.
B. Dua la kuku halimpati mwewe.
C. Kuku wa mkata hatagi.
D. Ng'ombe wa maskini hazai pacha.

25. Kielezi kilichopigiwa mstari ni cha aina gani?
**Sote tutaufanya mtihani wetu <u>mwakani</u>.**
A. Kielezi cha mahali B. Kielezi cha namna
C. Kielezi cha wakati D. Kielezi cha idadi

26. Chagua maelezo ambayo ni kweli.
A. Panda ni mnyama wa majini ilhali banda ni nyumba ambayo hutumika kuwekea wanyama
B. Kipepeo ni samaki mpana mwenye mapezi ya nyuma mapana, kipepeo pia ni mdudu.
C. Tembo ni mnyama mkubwa mwenye kipusa usoni, tembo pia ni aina ya kileo
D. Sahibu, shaibu, masaibu ni maneno yenye maana sawa.

27. Sentensi ipi iliyotumia kivumishi cha idadi katika orodha?
A. Darasa la pili lina wanafunzi wenye nidhamu.
B. Mwanafunzi ana madaftari manne.
C. Chakula kingi kimepelekewa mayatima.
D. Wezi wamerudisha pesa zote.

28. Tegua kitendawili:
**Huku ng'o na kule ng'o.**
A. umaskini B. njaa
C. giza D. mvua

29. Teua alama ya uakifisho inayotumika kutanguliza orodha.
A. ; B. -
C. ... D. :

30. Jibu gani **lisilolingana** na mengine?
A. Pole B. Samahani
C. Kunradhi D. Kumradhi

***<u>Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 31 to 40.</u>***

Nini ambacho kinajulikana ulimwenguni kote? Wengine watadai kuwa ni chumvi. Baadhi ya watu ama hata wote wanaweza wakasema kuwa ni pesa. Je, yawezekana binadamu yeyote ajulikane kila mahali kama pesa au chumvi? Ingawa Mzee Mvinyo hajulikani kote ulimwenguni, wakazi wote wa kaunti ya mamboleo wanamjua sio kwa jina tu bali pia kwa matendo yake. Walimu hawakosi kumtaja madarasani wanapofunza methali zinazolenga madhara ya kutotii. Si ajabu kuwapata baadhi ya waandishi wakitoa ulinganisho kuwa mlevi kama mzee Mvinyo. Aisee, Mzee Mvinyo alikuwa mlevi wa chupa na vizibo vyazo. Kila wakati alikuwa kalewa chakari, hata wengine wakafanya utani kuwa **alikuwa ameolewa na pombe**.

Asubuhi moja mbichi ilimshuhudia Mvinyo akichapua miguu kama panya aliyemwona paka kuelekea kwa Bwana Mapesa, tajiri aliyekuwa na pesa chungu nzima kama mchanga wa bahari. Bwana Mapesa alikuwa amenunua takribani shamba lote la mzee Mvinyo. **Pesa zote alizopewa nazo zilipulizwa na upepo wa pombe**. Licha ya kupokezwa mabunda ya noti siku baada ya siku, Mvinyo alisalia kuwa maskini nyasi asiye na mbele wala nyuma. Asubuhi hiyo alikuwa na nia ya kuuza kipande kidogo cha ardhi kilichosalia, ambapo kijumba chake cha msonge kiliinama kwa huzuni, majozi na jitimai. Alipofika langoni, alimwomba bawabu kipande cha sigara angaa **atulize kiu ya mwongo wa siku**.

Mvinyo alijipweteka kwenye kochi kubwa lililopambwa kwa matakia manene na foronya za kupendeza. Aliyapumbaza macho yake kwa kutazama taarifa za habari za siku iliyotangulia. Ghafla kama mawingu, aliona habari ambazo zilimshangaza nusura azimie. Aliona sherehe za ushindi wa kijana mmoja wa kike katika mashindano ya riadha. Mshindi huyo wa mbio za masafa marefu alipokezwa hundi ya shilingi milioni kumi kwa ubingwa wake. Mama na ndugu wa mwanariadha huyo walikuwa pale huku wamegubikwa gubigubi na furaha ya meno kutouma mkate.

"Ala! Ninaota au macho yangu yananichezea shere?" Mvinyo alijisaili huku akiyafikicha macho. Ukweli usiopingika ni kuwa hakuwa ndotoni wala hakuhadaiwa na macho yake. Aliyekuwa akizawidiwa alikuwa binti yake, nao waliokuwa wameandamana naye walikuwa mkewe na wanawe wengine. Mvinyo alikumbuka jinsi tamaa ilivyomshauri kumwoza binti yake. Tayari alikuwa amepokea kiasi fulani cha mahari. Binti huyo naye **hakuchelea** kuwaarifu walimu ambao walitishia kumripoti mzee Mvinyo katika kituo cha polisi. Juhudi za kumwoza binti yake zilipogonga mwamba, alianza mikakati ya kuliuza shamba lake ili alipe deni la mahari aliyopokezwa pamoja na kufurahia **utamu** wa **pombe**. Mkewe aliipinga hatua hiyo kwa jino na ukucha. Maji yalipozidi unga, alifunganya virago vyake kisha akaondoka pamoja na wanawe na kuguria kusikojulikana.

Mzee Mvinyo alikurupuka kutoka chumbani mwa mwenyeji wake kama mbwa aliyebumburushwa na chatu. Hakuona tena haja ya kuzungumza na mwenyeji wake. Alikuwa na jukumu muhimu sana la kutekeleza.

"Sina budi kuitafuta familia yangu. Ni lazima kama ibada tuishi pamoja kulingana na kudura zake mwenyezi Mungu." Mvinyo alijiambia pale njiani huku akiirusha mikono hewani kama mwehu. Alianza juhudi za kuitafuta aila yake ili aiombe msamaha. Alikuwa tayari kuuacha ulevi ima fa ima. Alikuwa tayari kuzirekebisha tabia zake. Naam! Alikuwa tayari.

**31.** Kulingana na aya ya kwanza, ni kweli kuwa Mzee Mvinyo;
A. alijulikana kote ulimwenguni
B. huwataja walimu darasani anapofunza
C. hutolewa ulinganisho na waandishi wote
D. alipenda pombe na kulewa kila wakati

**32.** Maneno **alikuwa ameolewa na pombe** yana maana kuwa
A. yeye na pombe walipendana sana.
B. mke wake alikuwa ametoroka.
C. alizoea kunywa pombe kila wakati.
D. pombe ilikuwa kama mke.

**33.** Kulingana na aya ya pili, ni kweli kuwa
A. Mzee Mvinyo alikuwa maskini kutokana na ulevi wake.
B. Mzee Mvinyo alienda kwa Bwana Mapesa kila siku asubuhi.
C. Bwana Mapesa alikuwa na deni la Mzee Mvinyo.
D. Mzee Mvinyo alikuwa ameuza hata nyumba yake.

**34.** **Pesa zote alizopewa nazo zilipulizwa na upepo wa pombe** ndiko kusema kuwa
A. pesa zote ziliibwa na pombe.
B. pesa zote ziibiwa na walevi.
C. alizitumia pesa zote kununua pombe.
D. upepo ulipuliza pesa zake zikapotea.

**35.** Kwa nini taarifa ambazo Mzee Mvinyo aliziona kwenye runinga zilishangaza?
A. Alishangazwa na ukubwa wa runinga.
B. Alishangazwa na msichana aliyekuwa akituzwa kwa kuwa alimfahamu.
C. Hakutarajia msichana huyo atunzwe siku hiyo.
D. Hakutarajia taarifa za habari zisomwe wakati huo.

**36.** **'... atulize kiu ya mwongo wa siku'** huku ni kusema kuwa alikuwa amekaa kwa siku muda gani bila kuvuta sigara?
A. Siku tano B. miezi kumi
C. miaka kumi D. siku kumi

**37.** Katika aya ya nne, walimu waliwajibika kwa njia gani?
A. Kumripoti mzee Mvinyo katika kituo cha polisi.
B. Kumlipia binti wa Mzee Mvinyo karo ya shule.
C. Kumtisha Mzee Mvinyo ili asimwoze binti yake.
D. Kumkanya Mzee Mvinyo asiuze shamba lake.

**38.** Neno **hakuchelea** lina maana gani jinsi lilivyotumika katika kifungu?
A. Kawia B. Zingatia
C. Kosa D. Ogopa.

**39.** Kwa nini mwandishi anatumia maneno **'utamu' wa pombe**? Inamaanisha kuwa;
A. haamini kuwa pombe ni tamu.
B. haujui utamu wa pombe.
C. anasisitiza utamu wa pombe.
D. hana matumaini na utamu wa pombe.

**40.** Kisa hiki kina funzo lipi kuu?
A. Tunafaa kuithamini elimu.
B. Ni vyema tuyathamini mashamba yetu.
C. Ni muhimu kuwathamini watoto wetu.
D. Ni bora kuthamini afya yetu.

***<u>Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali kutoka swali la 41 mpaka 50.</u>***

Katika uumbaji wa Mungu, aliamua katika busara na hekima yake kuumba vitu, watu, wanyama na kadhalika. Viumbe wote wa Mungu wana manufaa katika mazingira yetu. Hata wadudu ambao baadhi ya watu hudhani kuwa hawana faida wana umuhimu wao. Utagundua kuwa wapo wadudu ambao ni chakula cha wanyama wengine. Je, kuna tofauti ipi kati ya binadamu na wanyama au viumbe wengine? Licha ya kuwa kuna tofauti nyingi za kimaumbile na hata kimawazo, tofauti kubwa iliyo ni ubinadamu. Ubinadamu ni hali ya utambuzi wa jinsi ya kutekeleza wajibu juu ya maisha katika jamii. Ubinadamu pia huitwa utu. Pengine hii ndiyo sababu waambao huamba kuwa mtu ni utu.

Jambo la kwanza, ubinadamu huweza kudhihirika kupitia heshima. Heshima ni muhimu kiasi kuwa wazee wa kale walitushauri kuwa heshima si utumwa. Maneno ambayo mtu huyatumia yanaweza yakatumika kuwa **mizani** ya kiwango chake cha heshima. Maneno kama vile samahani, pole, asante na simile yanafaa kudumu kinywani mwa kila binadamu ambaye ni razini. Mavazi yako pia ni kigezo cha kutathmini heshima. Ingawa tunashauriwa kuwa **tusizingatie jinsi kitu kifananavyo nje kuamua ikiwa ni kizuri au kibaya**, ni bayana kuwa mavazi hutegemea kiwango cha mtu cha heshima. Yapo mavazi ambayo huwa mafupi mno, mengi hubana kupita kiasi, **mengine hukataa katakata kufunika sehemu muhimu** za mwili ilhali mengine hupwaya nusuru yaanguke.

Ukweli wa kauli kuwa wema hauozi, haufai kumtoka binadamu yeyote. Kila mara, hatukosi watu walio katika hali fulani ya uhitaji. Daima kunao marafiki, majirani au hata ajinabi ambaye

anahitaji msaada. Kuwafaa watu kama hao ndiko kutenda wema. Huo ndio ukarimu. Hakikisha maishani kuwa unapanda mbegu za wema kila uchao. Mtu yeyote ambaye ana upungufu wa kimaumbile kama vile upofu, ububu au ulemavu wowote anafaa kuonyeshwa matendo ya utu. Matendo ya utu ni kama vile kumwonyesha mtu njia, kumvusha asiyejiweza njia, kumsaidia mtu kuubeba mzigo, kumnunulia mtu chakula na kumpa mwingine mavazi. Matendo ya aina hii hufanyiwa mtu bila kutarajia malipo yoyote kutoka kwake.

Hatimaye, ubinadamu kamili humhitaji mtu kuwa mwenye bidii. Pengine umegundua kuwa baadhi ya misahafu hufundisha kuwa Mungu alifanya kazi kwa siku sita kisha akapumzika siku ya saba. Kimsingi, hili linafaa kuwa funzo kuwa muda mrefu wa maisha yetu utumiwe kufanya kazi. **Kulaza damu** ni tabia ambayo haifai hata kidogo. Wewe hulala kwa muda gani? Wewe hutazama runinga au kupiga gumzo kwa saa ngapi? Kuzembea ni tabia ambayo haionyeshi utu wala ubinadamu. Hebu fikiria kumhusu mchwa ambaye huweza kujenga kichuguu kikubwa bila kulazimishwa na mtu yeyote. Nyuki naye je, huweza kujenga sega na kutengeneza asali ambayo huufaa ulimwengu wote. Kati yake na mchwa au nyuki ni yupi mwenye akili au ubongo kuliko mwingine? Kwa hivyo, ni jambo la aibu mno kumwona binadamu akiwa mvivu na kukataa kufanya kazi. **Ikiwa mdudu kama vile mchwa anajua umuhimu wa kufanya kazi, sembuse binadamu**?

**41.** Aya ya kwanza inadokeza kuwa wadudu;
A. hawana faida yoyote ingawa hudhaniwa na baadhi ya watu kuwa wana faida.
B. huwa chakula cha wanyama wengi.
C. wana faida licha ya kudhaniwa na baadhi ya watu kuwa hawana faida.
D. wanajulikana kuwa hawana faida kwa maumbile.

**42.** Makala yanaeleza kuwa
A. tofauti kubwa iliyoko kati ya binadamu na wanyama ni akili.
B. kuna tofauti moja tu kati ya binadamu na wanyama.
C. tofauti nyingi kati ya binadamu na wanyama ni za kimaumbile.
D. ubinadamu ndio unaomtofautisha binadamu na wanyama.

**43.** Maneno **tusizingatie jinsi kitu kifananavyo nje kuamua ikiwa ni kizuri** yanaweza kuelezwa kwa methali ipi?
A. uzuri wa kuyu ndani mabuu.
B. Baniani mbaya kiatu chake dawa.
C. Kifo cha wengi harusi.
D. Usiache mbachao kwa msala upitao

**44.** Kifungu kinaeleza kuwa **mavazi mengine hukataa katakata kufunika sehemu muhimu**. Hii ni fani gani ya lugha?
A. Istiara B. Tashhisi
C. Chuku D. Kinaya

**45.** Aya ya tatu inadokeza kuwa;
A. kila mara tunakosa watu walio katika uhitaji.
B. tunafaa kuwaonyesha watu walio na upungufu matendo ya utu.
C. tuhakikishe kuwa tunapanda mbegu kila uchao.
D. matendo ya wema hufanyiwa mtu bila kutarajia.

**46.** Nahau **kulaza damu** ina maana gani jinsi ilivyotumika katika kifungu?
A. Kuwa mzembe.
B. Kulala sana.
C. Kumtoa mtu damu.
D. Kukosa utu.

**47.** Kulingana na aya ya mwisho, kwa nini Mungu alifanya kazi kwa siku sita na kupumzika siku moja?
A. Ili amfundishe binadamu umuhimu wa bidii
B. Ili asishindwe kukamilisha kazi yake.
C. Ili amalize kuumba viumbe wote.
D. Ili asipumzike kwa siku nyingi

**48.** Kwa nini mwandishi anatoa mifano ya mchwa na nyuki katika kifungu hiki?
A. Mchwa na nyuki ni wadudu muhimu.
B. Mchwa na nyuki hutumia akili kuliko binadamu.
C. Mchwa na nyuki ni mfano bora wa wadudu wenye bidii.
D. Mchwa na nyuki huandaa chakula kitamu kwa viumbe wengine.

**49.** **Ikiwa mdudu kama vile mchwa anajua umuhimu wa kufanya kazi, sembuse binadamu**? Huku ni kusema kuwa;
A. binadamu hana uwezo mwingi sawa na wa wadudu.
B. binadamu anatarajiwa kufanya kazi kwa bidii kuliko wadudu.
C. mchwa hatarajiwi kufanya kazi yenye manafaa.
D. mchwa hafai kujua umuhimu wa kazi.

**50.** Kifungu hiki kinaeleza mambo yafuatayo **isipokuwa**
A. heshima.
B. wema.
C. utamaduni.
D. juhudi.